# FIDIA eNEWSLETTER

TOLEO LA KUMI | JANUARI-MACHI 2026 | www.wcf.go.tz



# THAMANI YA WCF YAONGEZEKA

Karibu Sana

## YALIYOMO:


- Thamani ya WCF Yaongezeka
- WCF Yaelekezwa Kuweka Mikakati Madhubuti Kutekeleza Dira ya 2050
- WCF Yaimarisha Afya ya Watoto Wenye Uhitaji kwa Msaada wa Bima Dodoma
- Madaktari Wahimizwa kuwa Chachu katika Kuwahudumia Wafanyakazi Wanaopata Madhila Kazini


Jarida Mtandaoni
Skani Kodi ya QR
Hapo Chini


TIMU YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Dkt. John K. Mduma

MHARIRI MKUU
Laura G. Kunenge

MHARIRI MSAIDIZI
Sophia F. Mtakasimba

WACHANGIAJI
Mcharo S. Mrutu
Meseka Z. Kadala
Lilian R. Shembilu
Nuru A. Mwakivuma



# Dibaji

## Neno Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu

Karibuni katika toleo letu la kwanza la mwaka 2026. Kipindi hiki kinatupa fursa ya kutathmini tulikotoka na kujiwekea mwelekeo thabiti unaoendana na falsafa ya kazi na utu.

Katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), tunaendelea kusimamia kwa dhati misingi ya haki, uwajibikaji na uadilifu katika utoaji wa huduma. Kila tunachokifanya kinaakisi thamani ya maisha ya mwanadamu; kwamba nyuma ya kila huduma tunayotoa kuna hadhi na heshima ya mtu inayopaswa kulindwa na kuthaminiwa.

Katika kuimarisha mawasiliano na wadau, jarida hili linaendelea kuwa chombo muhimu cha kujenga uelewa kwa umma kuhusu majukumu, huduma na mafanikio ya WCF. Kupitia jarida hili, tunashirikisha maarifa, uzoefu na mwelekeo wa taasisi, kwa lengo la kuwawezesha wafanyakazi, waajiri na jamii kwa ujumla kufahamu vyema haki zao pamoja na namna bora ya kunufaika na huduma zetu. Tunaamini kuwa uelewa huu ni msingi imara wa ushirikiano wenye tija.

Aidha, tunaendelea kuboresha mifumo na huduma zetu ili ziwe rafiki zaidi, zenye uwazi na zinazokidhi matarajio ya wadau wetu. Dhamira yetu ni kuhakikisha kila mhudumiwa anapata haki yake kwa wakati na kwa heshima anayostahili.

Tunawashukuru wadau wote kwa ushirikiano wanaotupa, ushirikiano huu ni nguzo muhimu katika kutimiza wajibu wetu wa kuendeleza ustawi wa wafanyakazi nchini.

**Dkt. John K. Mduma**

# THAMANI YA WCF YAONGEZEKA




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu akizungumza wakati akifungua Mkutano wa Tano wa Baraza la Tatu la Wafanyakazi wa WCF.*

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu amepongeza jitihada zinazofanywa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) katika kutekeleza majukumu yake, hatua iliyochangia ukuaji wa Mfuko huo na kufikia thamani ya shilingi bilioni 844.41 mwezi Desemba 2025 kutoka shilingi bilioni 333.46 mwezi Juni 2020.

Amesema mafanikio hayo yameufanya Mfuko kuwa imara zaidi na wenye uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mujibu wa Ripoti ya Tathmini ya Mifuko iliyofanywa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) mwaka 2022.

Mhe. Sangu aliyasema hayo Februari 18, 2026 mjini Morogoro wakati akifungua Mkutano wa Tano wa Baraza la Tatu la Wafanyakazi wa WCF, ambao pamoja na mambo mengine ulilenga kupokea na kujadili mpango wa bajeti ya Mfuko kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Alieleza kuwa mafanikio hayo yametokana na uwekezaji wenye tija uliofanywa na Mfuko katika maeneo mbalimbali, ikiwemo hati fungani za Serikali, makampuni binafsi, uwekezaji katika ardhi, hisa katika masoko ya mitaji, amana za benki pamoja na uwekezaji wa pamoja.

"Ukuaji wa thamani ya WCF umetokana na uwekezaji wenye tija uliofanywa na Mfuko, ambapo hadi kufikia Desemba 2025 thamani ya uwekezaji imeongezeka na kufikia shilingi bilioni 891.12. Haya ni mafanikio makubwa ambayo kwa namna moja ama nyingine Baraza hili limechangia," alisema Mhe. Sangu.

Aliongeza kuwa pamoja na mafanikio hayo, WCF imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kukusanya michango kutoka kwa waajiri na kulipa fidia kwa wafanyakazi wanaopata madhira wanapokuwa kazini. Hadi kufikia Desemba 2025, jumla ya waajiri 44,834 walikuwa wamesajiliwa na Mfuko, huku zaidi ya shilingi bilioni 124 zikitumika kulipa fidia kwa wafanyakazi waliopata madhira kazini.

Vilevile, Mhe. Sangu alitoa maelekezo kwa uongozi wa WCF kuhakikisha haki za msingi za wafanyakazi zinazingatiwa, ikiwemo kupandishwa vyeo kwa wakati, kupata likizo, mafunzo pamoja na motisha mbalimbali kwa uwazi na bila upendeleo. Pia amewataka wajumbe wa Baraza kuhakikisha wafanyakazi wanashirikishwa ipasavyo katika mipango ya Mfuko na kuhimiza uwajibikaji, ambao ni nguzo muhimu ya mafanikio katika sehemu yoyote ya kazi.

**Inaendelea...**



*Mkurugenzi Mkuu wa WCFna Mwenyekiti wa Baraza Dkt. John Mduma akizungumza wakati wa Mkutano wa Tano wa Baraza la Tatu la Wafanyakazi wa WCF*



*Mwakilishi wa Chama Cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) Bi. Sarah Rwezaura akizungumza wakati wa Mkutano wa Tano wa Baraza la Tatu la Wafanyakazi wa WCF*

Awali, akimkaribisha Mhe. Waziri, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, alisema Baraza limeendelea kuwa kiunganishi muhimu kati ya uongozi na watumishi na kuongeza kuwa katika kikao hicho cha siku mbili, ajenda kuu zitakazojadiliwa ni pamoja na mpango wa bajeti kwa mwaka 2026/2027, wasilisho la Sera ya Kinga ya Jamii, pamoja na kusikiliza na kujadili hoja mbalimbali za wafanyakazi.



*Baadhi ya wa Baraza la Wafanyakazi wa WCF kwenye picha ya pamoja na Mhe. Sangu*

**Inaendelea...**

*Matukio mbalimbali wakati wa kikao cha tano cha baraza la tatu la wafanyakazi wa WCF*

















# WCF YAELEKEZWA KUWEKA MIKAKATI MADHUBUTI KUTEKELEZA DIRA 2050



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu akizungumza na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya WCF.*

**Na Mwandishi Wetu**

Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) yaelekezwa kuweka mikakati thabiti ya kuanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kwa lengo la kuuwezesha mfuko huo kuchangia zaidi katika utoaji wa huduma bora pamoja na kuongeza uzalishaji wa ajira, hususani kupitia sekta binafsi. Akizungumza na wajumbe wa bodi hiyo jijini Dodoma hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu, alisema kuwa Serikali kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kuanzisha na kuimarisha mfumo jumuishi wa hifadhi ya jamii utakaohusisha pia sekta isiyo rasmi.

Alieleza kuwa utekelezaji wa dira hiyo utachochea uwekezaji katika miradi ya maendeleo, kupanua wigo wa ulinzi wa kijamii, na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania wengi.
Mhe. Sangu alibainisha kuwa kuanzia mwezi Julai mwaka huu, Serikali itaanza rasmi utekelezaji wa Dira ya 2050, ambapo katika sekta ya hifadhi ya jamii, kipaumbele kimewekwa katika kukuza uchumi jumuishi na kuongeza ajira kupitia mchango wa sekta binafsi.

Aidha, alisisitiza kuwa katika mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano, sekta binafsi inatarajiwa kuchangia asilimia 70 ya uwekezaji, jambo linaloifanya WCF kuwa na jukumu la kupanua wigo wa wanachama wake kutoka sekta binafsi ili kuongeza kiwango cha michango na kuimarisha uhimilivu wa mfuko.

"Ni muhimu kuitazama sekta binafsi kama mhimili mkuu wa kukuza uchumi. WCF inapaswa kubuni na kuwekeza katika miradi ya kimkakati itakayoongeza uzalishaji wa ajira na kuvutia wachangiaji wengi zaidi," alisisitiza Waziri Sangu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya WCF, Bi. Renata Rugarabamu, alimweleza Waziri kuwa mfuko huo unaendelea kuwa imara kifedha na unatoa huduma zake kwa wafanyakazi kwa weledi, ufanisi na ubora unaokidhi matarajio ya wanufaika. Aidha, aliahidi kuwa Bodi ya Wadhamini itatekeleza kikamilifu maelekezo yote yaliyotolewa na Mhe. Waziri, ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kuendana na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.



*Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya WCF wakifuatilia kikao*




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu akiwa kwenye picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya WCF.*

# WCF YAIMARISHA AFYA YA WATOTO WENYE UHITAJI KWA MSAADA WA BIMA DODOMA

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetoa msaada wa bima ya afya kwa watoto 162 wanaolelewa katika Makao ya Taifa ya Kulelea Watoto yaliyopo Kikombo jijini Dodoma, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wake wa kurejesha kwa jamii (CSR) unaolenga kusaidia makundi yenye uhitaji.




*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Rahma Riyadh Kisuo akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi msaada wa bima ya afya kwa watoto wanaolelewa katika Makao ya Taifa ya Kulelea Watoto yaliyopo Kikombo jijini Dodoma hivi karibuni.*

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi kadi hizo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Rahma Riyadh Kisuo, aliipongeza WCF kwa kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa makundi mbalimbali ya jamii.
Mhe. Kisuo alisema msaada huo wa bima ya afya wa mwaka mmoja unaonesha namna ambavyo WCF inajali si tu wafanyakazi tu ambao ni wadau wake wakuu, bali pia familia zao na jamii inayowazunguka.

Alieleza kuwa hatua hiyo inaunga mkono kwa vitendo juhudi za Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha ustawi, malezi na afya za watoto, sambamba na kuendeleza azma ya kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma za bima ya afya kupitia Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

"Hakika mmeonesha kuwa hamuishii kuwahudumia wafanyakazi pekee, bali pia mnajali jamii kwa ujumla, wakiwemo watoto hawa. Huu ni mfano bora wa kuigwa na taasisi nyingine," alisema Mhe. Kisuo.




*Mhe. Kisuo (Kulia) na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Maryprisca Mahundi (Kushoto) wakionyesha mfano wa kadi ya bima ya afya zilizotolewa kwa watoto wa Kikombo.*

Aidha, aliwataka wadau wengine, ikiwemo taasisi na mashirika mbalimbali, kuanzisha na kuimarisha mipango ya kurejesha kwa jamii kwa kutoa misaada katika sekta muhimu kama afya na elimu, hasa kwa makundi yenye uhitaji.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Maryprisca Mahundi, aliunga mkono kauli hiyo kwa kusema kuwa WCF imeendelea kuwa mdau muhimu wa wizara hiyo kutokana na mchango wake katika kusaidia makundi mbalimbali, wakiwemo wanawake, wazee, watoto na vijana.

Awali, akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema sekta ya afya ni miongoni mwa maeneo yanayopewa kipaumbele na mfuko huo kupitia sera yake ya kurejesha kwa jamii, kwa lengo la kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya.

Alibainisha kuwa WCF itaendelea kushirikiana na Serikali na wadau wengine katika kuboresha ustawi wa jamii, hususani kwa makundi yenye uhitaji, ili kujenga taifa lenye afya bora na nguvu kazi yenye tija.

# WCF YAIMARISHA AJIRA KWA VIJANA KUPITIA KILIMO CHA CHAI LUSHOTO

**Na Mwandishi Wetu**

Vijana nchini wameaswa kuchangamkia fursa zinazotokana na uwekezaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) katika mnyororo wa thamani wa zao la chai, kupitia Kiwanda cha Chai cha Mponde, ili kujenga ajira endelevu na kipato cha uhakika.

Wito huo umetolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii wakati wa ziara yake katika Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, ambapo imeeleza kuwa uwekezaji wa WCF unalenga si tu kuongeza uzalishaji bali pia kuwawezesha vijana kujiajiri na kushiriki kikamilifu katika uchumi wa viwanda.

Akizungumza Machi 14, 2026 katika Kiwanda cha Chai cha Mponde, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hawa Mchafu, alisema uwepo wa kiwanda hicho unatoa jukwaa muhimu kwa vijana kujifunza, kuajiriwa na hata kuanzisha mashamba ya chai kwa uhakika wa soko. "Kilimo cha chai kina mchango mkubwa katika kuzalisha ajira na kuongeza kipato kwa vijana, hususan pale wanapounganishwa na uwekezaji wa kimkakati kama huu wa WCF," alisisitiza.

Alibainisha kuwa kupitia uwekezaji huo wa ubia kati ya WCF na PSSSF, jamii inayozunguka kiwanda inanufaika kwa kupata ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, huku vijana wakipewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji, usindikaji na usambazaji wa zao hilo.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano, Deus Sangu, alisema uwekezaji huo unaendana na juhudi za Serikali za kukuza ajira kwa vijana na kuimarisha uchumi wa viwanda. Alieleza kuwa kiwanda hicho kinazalisha na kuuza chai katika masoko ya ndani na nje ya nchi, jambo linaloongeza thamani ya zao hilo na kupanua fursa kwa vijana kushiriki katika biashara ya kimataifa.

Ziara hiyo imeonesha dhahiri dhamira ya WCF ya kuendelea kuwekeza katika miradi yenye tija inayolenga kuinua vijana kiuchumi, kuongeza ajira na kuchochea maendeleo jumuishi nchini.

*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii wakijionea hatua mbalimbali za uchakataji wa zao la Chai, katika Kiwanda cha Chai Mponde*







# MADAKTARI WAHIMIZWA KUWA CHACHU KATIKA KUWAHUDUMIA WAFANYAKAZI WANAOPATA MADHILA KAZINI.

**Na Mwandishi Wetu**

Madaktari nchini wamehimizwa kuwa chachu ya maboresho katika kuwahudumia wafanyakazi wanaopata changamoto kutokana na kazi zao ili kulinda nguvu kazi ya taifa na kuongeza tija katika utendaji kazi.

Wito huo umetolewa Machi 24, 2026 na Mkuu wa Wilaya ya Singida Mjini Mhe. Godwin Gondwe aliyemuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendegu kwenye ufunguzi wa mafunzo ya tathmini za ulemavu unaosababishwa na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari wa mikoa ya Singida, Tabora, Dodoma, Kigoma, Manyara na Shinyanga.



*Mkuu wa Wilaya ya Singida Mjini Mhe. Godwin Gondwe wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya tathmini za ulemavu unaosababishwa na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari wa mikoa ya Singida, Tabora, Dodoma, Kigoma, Manyara na Shinyanga.*

Mafunzo hayo yaliendeshwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati wake wa kuwajengea madaktari uelewa wa taratibu za kuwahudumia wanufaika wa WCF, kuongeza uwezo wa kutambua magonjwa yatokanayo na kazi, pamoja na kuwaimarishia uwezo wao wa kufanya tathmini ya athari za kibaiolojia zitokanazo na ajali au magonjwa ya kikazi.

Mhe. Gondwe aliwaeleza madaktari wanaoshiriki kwenye mafunzo hayo kuwa ili WCF iweze kutoa fidia stahiki kwa walengwa inawategemea sana wao kwa namna watakavyoweza kuwahudumia wafanyakazi waliopata ajali au ugonjwa unaotokana na kazi pamoja na kufanya tathmini za ulemavu kwa usahihi na kwa wakati.

“Ni matarajio ya Mfuko na Serikali kuwa kupitia utendaji wenu bora, wafanyakazi wenye changamoto watarejea kazini mapema, tathmini za ulemavu zitafanyika kwa wakati na fidia stahiki zitatolewa kwa wakati na kwa usahihi. Hivyo, ninawasihi mtumie mafunzo haya kuongeza uelewa wenu kuhusu taratibu za WCF, utambuzi wa magonjwa ya kazi, na mbinu sahihi za tathmini ya ulemavu na hatimaye kulinda na kuendeleza nguvu kazi ya taifa letu,” alisema Mhe. Gondwe.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma alieleza kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya kuboresha na kusogeza huduma za Mfuko karibu na walengwa.

“Mafunzo haya ni sehemu ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Mfuko hususani katika kuhakikisha wanufaika wanapata huduma bora za matibabu na tathmini sahihi na kwa wakati wanapopata ajali au magonjwa yatokanayo na kazi,” alisema Dkt. Mduma.

Mafunzo hayo yalihudhuriwa na madaktari wapatao 120 kutoka ngazi za vituo vya afya hadi hospitali za rufaa kutoka mikoa ya Singida, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Manyara na Kigoma.




*Mhe. Godwin Gondwe na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Dkt. John Mduma.*

**Inaendelea...**

## *Matukio mbalimbali wakati wa mafunzo ya madaktari mkoani Singida*











# RUFAA ZA MAAMUZI YA WCF ZAPUNGUA -WAZIRI SANGU

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umepongezwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano ya Kazi, Mhe. Deus Sangu, kwa utendaji mzuri uliosababisha kupungua kwa rufaa za walalamikaji wanaokuwa hawajaridhika na maamuzi ya WCF na kuwasilisha rufaa zao kwa Waziri mwenye dhamana ya kazi kwa mujibu wa sheria. Hatua hiyo inaonesha kuimarika kwa utoaji wa haki na ufanisi wa mifumo ya kushughulikia madai kwa wanufaika.

Waziri alitoa pongezi hizo jijini Arusha tarehe 9 Februari, katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Arusha (AICC), alipotembelea banda la WCF wakati wa Mkutano Mkuu wa Wadau wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, uliokwenda sambamba na uzinduzi rasmi wa Sera ya Kinga ya Jamii.

Akizungumza katika banda la WCF, Mhe. Waziri Sangu alisema kuwa kupungua kwa rufaa ni kiashiria cha maboresho makubwa yaliyofanywa na WCF katika utoaji wa huduma, ikiwemo kuimarisha mifumo ya uchakataji wa madai, kuongeza uwazi, na kuzingatia misingi ya haki kwa wafanyakazi waliopata madhila kazini.

"Napenda kuipongeza WCF kwa kazi nzuri wanayoifanya. Takwimu zinaonesha wazi kuwa rufaa za walalamikaji ambao hawajaridhika na maamuzi yenu na kuja kwangu zimepungua, jambo linaloashiria kuwa WCF inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa kuzingatia misingi ya haki," alisema.

Aidha, Waziri alisisitiza kuwa mafanikio hayo yana mchango mkubwa katika kuimarisha imani ya wananchi kwa mifuko ya hifadhi ya jamii na yanaunga mkono azma ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata kinga ya kijamii iliyo jumuishi na endelevu.

Akimkaribisha Waziri katika banda la WCF, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alimueleza Mhe. Waziri Sangu kuwa kati ya mafao saba yanayotolewa na mfuko huo, mojawapo ni fao la utengamao, linalolenga kumrejesha mfanyakazi aliyepata madhara kazini yaliyosababisha ulemavu ili aweze kurejea katika jamii na kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi.




Inaendelea...

“WCF inatekeleza fao la utengamao linalotolewa kwa misingi ya kitabibu, kijamii na kiufundi. Lengo lake kuu ni kumrejesha mfanyakazi aliyepata madhila kazini aweze kuchangamana na jamii na kuendelea na maisha ya kawaida,” alieleza Dkt. Mduma.



Akizindua Sera ya Kinga ya Jamii ya Mwaka 2025, Mhe. Waziri Sangu alitoa wito kwa taasisi zote za hifadhi ya jamii kuendelea kuboresha huduma, kuimarisha mifumo ya kidijitali, na kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali ili kufanikisha utekelezaji wa malengo ya sera hiyo mpya.

Mkutano huo uliwakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya hifadhi ya jamii, wakiwemo viongozi wa Serikali, mifuko ya hifadhi ya jamii, waajiri, vyama vya wafanyakazi na wadau wa maendeleo, kwa lengo la kujadili mwelekeo wa sekta hiyo na mchango wake katika ustawi wa jamii na maendeleo ya taifa.








Inaendelea...

***Matukio mbalimbali wakati wa uzinduzi wa sera ya taifa ya kinga ya jamii na mkutano mkuu wa wadau wa sekta ya kinga ya jamii***



















# WCF YAIBUKA KIDEDEA MAONESHO YA HUDUMA ZA FEDHA



*Mkuu wa Mko wa Tanga Mhe. Balozi. Dkt. Batilda Buriani akimkabidhi tuzo Afisa Uhusiano Mkuu wa Mfuo wa Fidia kwa Wafanyakazi Bw. Mcharo Mrutu wakati wa kilele cha Maonesho ya Wiki ya Fedha 2026*

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeibuka mshindi wa pili katika kipengele cha Hifadhi ya Jamii katika kilele cha Maonesho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa 2026, yaliyokuwa yakifanyika jijini Tanga.

Ushindi huu unatokana na utoaji wa huduma bora kwa wadau waliokuwa wakitembelea banda la Mfuko wakati wote wa maonesho hayo.

Maonesho hayo yamehitimishwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian, ambaye alipongeza WCF kwa jitihada zao za kutoa fidia stahiki kwa wakati, pamoja na elimu endelevu kwa wananchi, waajiri na wafanyakazi kuhusu taratibu za madai ya fidia, uwasilishaji wa michango kwa wakati, na sheria zinazolinda wafanyakazi.





# WCF NA JESHI LA POLISI WAIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA USHUGHULIKIAJI WA AJALI ZA WAFANYAKAZI

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Jeshi la Polisi Tanzania wamefanya kikao kazi mjini Morogoro hivi karibuni, kilicholenga kuimarisha ushirikiano katika ukusanyaji na uthibitishaji wa taarifa muhimu za ajali za wafanyakazi, hatua inayolenga kuboresha utoaji wa huduma na kuhakikisha haki za watumishi zinatimizwa kwa wakati.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Kamishna wa Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi wa Jeshi la Polisi Tanzania Bw. Shabani Hiki, alisisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na WCF.

"Jeshi la Polisi lina jukumu muhimu la kutoa nyaraka na vielelezo vya matukio ya ajali, ambavyo hutumika kama msingi wa kuchakata na kuidhinisha madai ya fidia kwa wafanyakazi waliopata madhira wakiwa kazini"alisema kamishna Hiki.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema kikao hicho kililenga kuweka mikakati ya kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili, kuhakikisha mchakato wa madai unafanyika kwa haraka, kwa uwazi na kwa kuzingatia haki za wafanyakazi.

Dkt. Mduma aliongeza kuwa WCF itaendelea kushirikiana kwa karibu na Jeshi la Polisi katika kuboresha mifumo ya mawasiliano na uratibu, ili nyaraka muhimu za ajali zipatikane kwa wakati na kwa ubora unaohitajika.

Pande zote mbili zilikubaliana kuendeleza ushirikiano huo kwa njia ya kuboresha upatikanaji wa taarifa, kubadilishana uzoefu, na kutoa mafunzo kwa wadau, ili kuongeza uelewa wa pamoja kuhusu taratibu za kushughulikia ajali za wafanyakazi.

Hatua hii inatarajiwa kuongeza ufanisi katika kushughulikia madai ya fidia na kuhakikisha wafanyakazi wanaopata madhila kazini wanapata haki zao kwa haraka na kwa usahihi.



*Kamishna wa Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi wa Jeshi la Polisi Tanzania Bw. Shabani Hiki na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Dkt. John Mduma.*



*Baadhi ya Watumishi wa WCF katika kikao kazi*


*Baadhi ya Watumishi wa Jeshi la Polisi katika Kikao Kazi*

# RC SENYAMULE AIPONGEZA WCF KWA HUDUMA NZURI




**Na Mwandishi Wetu**


Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, ameupongeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa juhudi zake katika kuhudumia wafanyakazi nchini.

Mhe. Senyamule alitoa pongezi hizo Machi 6, 2026 alipotembelea banda la WCF wakati wa maonesho ya mafanikio ya siku 100 za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan yalifanyika katika Uwanja wa Nyerere Square, jijini Dodoma, yakibeba kaulimbiu isemayo “Kero yako, wajibu wangu; Huduma Bora, Maisha Bora.”

Akiwa katika banda la WCF, Mhe. Senyamule alipatiwa maelezo kuhusu majukumu na huduma mbalimbali zinazotolewa na mfuko huo, hususan utoaji wa fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali au magonjwa yatokanayo na kazi. Pia alielezwa kuhusu juhudi zinazofanywa na WCF katika kuimarisha ustawi na usalama wa wafanyakazi nchini.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na waajiri kuhusu umuhimu wa kujiunga na mfumo wa fidia kwa wafanyakazi, akibainisha kuwa hatua hiyo inachangia kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi.

Sambamba na hilo, alisisitiza umuhimu wa taasisi za umma na sekta binafsi kuhakikisha changamoto za wananchi zinapatiwa ufumbuzi kwa haraka, ili kupunguza malalamiko na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.



# WAFANYAKAZI WANAWAKE WASHEREKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI









*Picha mbalimbali za wafanyakazi wanawake wa WCF walioshiriki Maadhimisho katika mikoa mbalimbali*

**Na Mwandishi Wetu**

Wanawake wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Machi 8 mwaka huu wameungana na wanawake wote duniani kuadhimisha Siku ya kimataifa ya Wanawake ambayo ilibeba kauli mbiu isemayo "Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana: Msingi Jumuishi kuelekea Dira 2050." Kupitia maadhimisho haya, wanawake wa WCF wameendelea kuonesha dhamira yao ya kusimamia usawa, uwezeshaji na maendeleo jumuishi kwa wanawake na wasichana wote

Sambamba na sherehe hizo, walipata fursa wametembelea na kuwajulia hali wagonjwa wanaoendelea kupata matibabu katika Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuwafariji.

Ziara hiyo ilelenga kuimarisha mahusiano kati ya WCF, ORCI na jamii kwa ujumla, kwa kuzingatia misingi ya falsafa ya Kazi na Utu, huku ikihamasisha mshikamano na uwajibikaji wa kijamii miongoni mwa taasisi na wadau mbalimbali.

**Inaendelea...**

## *Matukio mbalimbali wakati wa maadhimisho ya Siku ya wanawake*

















# WCF, NIT WAUNGANA KUKABILIANA NA AJALI BARABARANI, KAZINI.




*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. John Mduma na Mkuu wa  Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) Dkt. Prosper Mgaya wakisaini hati ya Makbubaliano.*

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) wamesaini rasmi Hati ya Makubaliano (MoU) yenye lengo la kuimarisha usalama barabarani na kupunguza ajali zinazohusiana na kazi nchini.

Akizungumza katika hafla ya kutia saini makubaliano hayo Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. John Mduma alisema kuwa ushirikiano huo ni hatua muhimu katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya mfuko huo, hususan katika kushughulikia changamoto ya ajali za barabarani ambazo zimekuwa chanzo kikubwa cha madai ya fidia kwa wafanyakazi.




*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. John Mduma na Mkuu wa  Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) Dkt. Prosper Mgaya wakionyesha hati ya makubaliano mara baada ya kuweka saini*

"Asilimia kubwa ya madai ya fidia yanayopokelewa WCF yanatokana na ajali za barabarani, zinazowahusisha madereva wa vyombo mbalimbali pamoja na wafanyakazi wanaotumia usafiri kwenda na kutoka kazini, hivyo kupitia makubaliano haya WCF na NIT zitashirikiana katika maeneo manne muhimu ambayo ni utoaji wa mafunzo na elimu ya usalama katika sekta ya usafirishaji, kufanya tafiti, kubadilishana taarifa, pamoja na kujengeana uwezo wa kitaalamu" Alieleza Dkt Mduma.

Kwa upande wake Mkuu wa  Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) Dkt. Prosper Mgaya alieleza kuwa kuwa tukio hilo linaashiria hatua muhimu katika juhudi za pamoja za kukabiliana na changamoto ya ajali za barabarani, ambazo zinaendelea kuwa tatizo kubwa na kwamba takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinazoonesha kuwa takribani watu milioni 1.19 hupoteza maisha kila mwaka duniani kutokana na ajali za barabarani, huku mamilioni ya wengine wakipata ulemavu wakudumu.

"Katika nchi zinazoendelea, ikiwemo Tanzania, ajali za barabarani hugharimu kati ya asilimia 3 hadi 5 ya Pato la Taifa (GDP) kutokana na kupotea kwa nguvu kazi, gharama za matibabu na fidia pamoja na athari nyingine za kiuchumi"

Kwa pamoja, WCF na NIT zimeahidi kuimarisha ushirikiano huo ili kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa makubaliano hayo, kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani, kulinda nguvu kazi ya taifa na kuimarisha ustawi wa jamii kwa ujumla




**Inaendelea...**

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA















# PICHA ZA MATUKIO MBALIMBALI



# TANGAZO

## TARATIBU ZA KUWASILISHA MADAI ENDAPO MFANYAKAZI ATAPATA UGONJWA, AJALI AU KIFO KINACHOTOKANA NA KAZI

1. Mwajiriwa au mtu yeyote atatoa taarifa kwa mwajiri wake mapema tokea tukio la ajali lilipotokea .
2. Mwajiri ataripoti ajali hiyo kupitia mfumo wa ONS(Online notification system) akiwa na taarifa kamili ya ajali (Majina kamili na namba ya simu ya mfanyakazi aliepata ajali hiyo)

3. Mwajiri atalazimika kujaza fomu iliyopo kwenye mfumo (WCN-1) mapema baada ya kukamilisha kujaza taarifa ya ajali hiyo kwenye mfumo wa WCF Mwajiriwa ambaye amepata ajali hiyo atapokea ujumbe Kwenye namba yake ya simu kutoka WCF ukiwa na maelezo na namba ( WCF Notification Number) ya kutumia kwenye matibabu kwaajili ya matumizi.

4. Mfuko utamtaarifu Mwajiri na Mwajiriwa kuhusu kupokelewa au kukataliwa kwa taarifa ya tukio la ajali baada ya uhakiki.

Kwa Madai ya Ajali/Kifo Kilichosababishwa na Ajali: Mwajiri atafuata uwasilishaji wa madai kama ifuatavyo, hususani:
i)Mkoa/Wilaya ambayo mfanyakazi anafanya kazi
ii) Tukio limetokea sehemu gani mfano:
iii) Ndani ya eneo la kazi (on premises)
iv) Nje ya eneo la kazi (out of premises)
v) Wakati wa usafiri (conveyance)
vi) Taarifa za mtoa huduma za afya (HCP)
vii) Hali ya afya ya mfanyakazi aliyejeruhiwa
Ugonjwa/Kifo Kilichosababishwa na Ugonjwa
Nyaraka za lazima kabla ya kubofya "Notify" ni:
• Ripoti ya uchunguzi wa kitabibu (Medical Diagnosis Report)
• Mkataba wa ajira (Contract of Employment)
viii) Kwa taarifa zilizokubaliwa nyaraka zifuatazo zitalazimika kuwasilishwa;

a)Katika kipindi cha matibabu : Fomu zilizojazwa na daktari zinahitajika kwa ajili ya malipo ya fidia ya ulemavu wa muda ambazo ni (Ripoti ya awali ya matibabu WCC-2a, Ripoti ya Maendeleo ya matibabu WCP-3, Ripoti ya Daktari ya kufunga matibabu WCC-2B)

b)Endapo mwajiri au mwajiriwa wametumia gharama katika matibabu, watalazimika kuwasilisha risit na nyaraka zozote zinazoweza kuthibitsha madail ili kurudishiwa gharama hizo.

# WCF MKONONI APP




# PAKUA SASA

ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA